




MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

Na: 1. Msimu wa Kilimo 2019/20


Tathmini Septemba 21-30, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha Oktoba 1-10, 2019

Muhtasari

- Wakulima katika maeneo mengi ya nchi wanaendelea na kuandaa mashamba kwa ajili ya misimu ya mvua za Msimu na Vuli.
- Wakulima katika maeneo ya ukanda wa ziwa Viktoria, pwani ya kaskazini, pwani ya kusini na nyanda za juu kaskazini mashariki wanashauriwa kuendelea na maandalizi ya mashamba, mpaka kutakapokuwa na unyevunyevu wa kutosha kwenye udongo kwa ajili ya kupanda.
- Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua itasababisha upungufu wa maji na malisho ya mifugo, hivyo wakulima, wavuvi na wafugaji wanashauriwa kuzingatia matumizi endelevu ya maji na malisho.

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 21-30, 2019

Katika dikadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo eneo la kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika katika nusu ya kwanza ya kipindi hiki ikilinganishwa na ile iliyopo eneo la kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ambayo iliendelea kuimarika. Hali ya kuimarika kwa mgandamizo mkubwa wa hewa (Azore na St. Helena) ilipelekea kuendelea kuusogeza ukanda wima wa mvua maeneo yanayozunguka ukanda wa ziwa Viktoria. Hata hivyo, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo eneo la kusini mwa dunia iliimarika nusu ya mwisho ya kipindi hiki na hivyo kupelekea mkondo wa mgandamizo mkubwa wa hewa kusababisha upepo mkali maeneo ya ukanda wote wa pwani. Uwepo wa joto la bahari la juu kidogo ya wastani katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi liliendelea kusababisha mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani ya kaskazini hususan nusu ya pili ya kipindi hiki. Aidha, joto la bahari la juu kidogo ya wastani liliripotiwa katika maeneo ya pwani ya Angola.



Kielelezo 1: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Septemba 21- 30, 2019.

MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 21-30, 2019

Kwa kipindi hicho cha dikadi maeneo mengi ya nchi yalikuwa makavu isipokua kwa baadhi ya maeneo mengi ya ukanda wa Ziwa Viktoria isipokuwa mkoa wa shinyanga, mkoa wa Kigoma na pwani ya kaskazini hususan mkoa wa Tanga. Kiasi cha mvua kilichopimwa ni kati ya milimita 11 hadi milimita 100 inavyoonekana, kama inavyojieleza katika kielelezo.

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 21-30, 2019

Katika kipindi cha dikadi iliyopita wakulima katika maeneo mengi yanayopata mvua za vuli waliendelea na uandaaji wa mashamba isipokuwa katika mkoa wa Kagera ambapo wameanza kupanda mazao ya mahindi na maharagwe. Kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua wakulima wanaendelea na maandalizi ya mashamba kwa msimu wa kilimo unaotarajiwa kuanza mwezi Novemba na Disemba. Upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo ulikuwa wa wastani katika maeneo mengi ya

nchi, isipokuwa katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Mwanza, Mara, Simiyu, Shinyanga, Singida, Arusha, Manyara na Dodoma ambako hali ya maji na malisho iliendelea kupungua kuliko maeneo mengine ya nchi.

HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 21-30, 2019

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito viliendelea kupungua katika maeneo mengi ya nchi kutokana na hali ya ukavu inayoendelea.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 1-10, 2019

Katika dikadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo eneo la kusini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kudhoofika ikilinganishwa na ile iliyopo eneo la kaskazini mwa dunia ambayo inatarajiwa kuimarika. Hali hii inatarajiwa kuendelea kuusogeza ukanda wima wa mvua maeneo yanayozunguka ukanda wa ziwa Viktoria. Halikadhalika hali hii inatarajiwa kusababisha uwepo wa upepo wa kawaida na kuendelea kuusukuma ukanda wa mvua wa Kitropikali kutoka kaskazini kuelekea kusini mwa Ikweta. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani. Aidha, joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika maeneo ya pwani ya Angola.

HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 1-10, 2019

Maeneo ya kanda ya ziwa Viktoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) yanatarajiwa kupata mvua kiasi katika maeneo machache.

Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) na kanda ya kusini (mikoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kupata hali ya ukavu.

HALI YA KILIMO INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 1-10, 2019

Kuongezeka kwa kiwango cha unyevunyevu wa udongo kunatarajiwa katika maeneo ya ukanda wa ziwa Viktoria, pwani ya kaskazini, pwani ya kusini na nyanda za juu kaskazini mashariki kutokana na mvua zinazotarajiwa katika dikadi hii. Wakulima wanashauriwa kuzitumia mvua hizi kupanda pale kutakapokuwa na unyevunyevu wa kutosha kwenye udongo. Wakulima wanashauriwa kuendelea kuandaa mashamba kwa ajili ya msimu wa mvua za Vuli unaotarajiwa kuanza kati ya mwezi Novemba na Desemba. Wakulima, wavuvi na Wafugaji wanashauriwa kuchukua hatua stahiki kwa kuzingatia ushauri wa maafisa ugani katika maeneo yao.

HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 1-10, 2019

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuwa vya wastani katika sehemu nyingi nchini. Hata hivyo, wananchi wanashauriwa kutumia maji kwa uangalifu kwa matumizi endelevu ya rasilimali hii.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3-Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania